# Ufalme wa Mungu Ni Nini? (Sehemu ya 1)

Inategemea sura ya 8 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye www.jw.org/sw.

**LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo. Jifunze kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.**



## KWA NINI WATAWALA WA UFALME WA MUNGU WANASTAHILI KAZI HIYO?

### 1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Unafikiri watu wengine wangesema nini?

*Wewe* unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?



www.jw.org/sw © 2015 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

## 2 CHUNGUZA BIBLIA INAFUNDISHA NINI

### Yesu ni Mfalme bora.

( Tazama sura ya 8 ya kitabu *Biblia Inafundisha,* fungu la 1 hadi la 7.)

**Soma 1 Timotheo 6:15, 16.**

Mistari hiyo inaonyesha jinsi gani kwamba Yesu ataweza kufanya mambo mengi mazuri kuliko mtawala yeyote mwanadamu?

______________________________

______________________________

______________________________

**Soma Isaya 11:2-4.**

Unabii huu ulitaja nini kuhusu jinsi Yesu atakavyotenda akiwa mtawala?

______________________________

______________________________

______________________________



**Yehova amechagua wanadamu waaminifu wenye hali na malezi mbalimbali ili watawale pamoja na Yesu**



www.jw.org/sw © 2015 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

## Yehova amechagua watawala wanaoelewa vizuri hisia zetu.

( Tazama sura ya 8 ya kitabu *Biblia Inafundisha,* fungu la 8 hadi la 10.)

**Soma Ufunuo 5:10 na 14:1, 4.**

Kulingana na mistari hii, ni nani wengine watakaotawala pamoja na Yesu?

Tunajuaje kwamba wale watakaotawala na Yesu wanaelewa changamoto tunazokabili?
(Dokezo: Soma tena Ufunuo 14:4b; linganisha na 1 Wakorintho 6:9-11.)

Ni nini kinachokusadikisha kwamba Yesu na wale 144,000 wanastahili kutumika wakiwa watawala katika Ufalme wa Mungu?


www.jw.org/sw © 2015 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

## 3 ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

**Yesu aliishi na kufa maelfu ya miaka iliyopita. Hivyo, hatutapata faida yoyote tukifuata mambo aliyofundisha.**

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

**Huenda watu wengi watakubaliana na wazo hilo. Lakini ninaamini jambo tofauti na hilo kwa sababu . . .**

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?

MTU AKISEMA . . .

**Kuna malaika wengi mbinguni, hivyo sioni sababu yoyote ya watu 144,000 kuchaguliwa kutoka duniani.**

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

**Ni kweli kwamba kuna malaika wengi mbinguni. Lakini ninaamini kwamba kuna faida nyingi za kuwa na watawala wanadamu kwa kuwa . . .**

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?


www.jw.org/sw © 2015 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania